kustawisha amani. Mhindu atuulizapo kwamba ninyi mwamfahamuje Ram Chandar Ji, basi sisi twasema kwamba twamfahamu huyo kuwa ni mtakatifu wa Mwenyezi Mungu. Baada ya Mhindu kulisikia jibu hili anawezaje kutukasirikia. Vivyo hivyo popote pale tuendapo hatutakuwa na hofu ya jambo hili la kuwasema vibaya watakatifu wa wengine. Kama yeyote aseme kwamba aliwahi kupita mja fulani wa Mwenyezi Mungu katika eneo fulani la huko Amerika au Afrika, basi sisi tutasema; Sawa, kwani Kurani ilishatoa elimu hii tangu awali kwamba alipita katika kila kaumu mwongozi. Hivyo kwa njia ya fundisho hili, Mtume s.a.w. aliufungua mlango mmoja wa kustawisha amani.

“Sababu nyingine ya magomvi huwa ni hii kwamba mtu huwa hawasemi vibaya watakatifu wa kaumu zingine lakini huyasema vibaya mafundisho yao. Kwa njia ya Mtume s.a.w., Mwenyezi Mungu Amekizuia pia kitendo hiki. Mwenyezi Mungu Alitangaza kwa kumpitia yeye kwamba;

Hata msivitukane pia vitu vile vinavyoheshimiwa na watu wa dini zingine kama vile masanamu nk. Ingawa vitu hivyo hamvioni kuwa ni sahihi, lakini hata hivyo hamna haki ya kuvitaja kwa maneno makali, kwani kwa njia hii mioyo ya watu hao itaumia na kisha magomvi au fujo zitatokea nao pia, bila kutafakari, watayasema vibaya mafundisho yenu na kumtusi Mwenyezi Mungu kutokana na upinzani. Haya ni mafundisho ya juu kiasi gani aliyoyaleta Mtume s.a.w.. na wale watakatifu wa dini zingine waliokuwa wakweli, alisema, kuhusiana nao, kwamba waaminini na vile vilivyokuwa si vya kweli akasema kuhusiana navyo kwamba Msiviseme vibaya.”
Karibuni tujiunge na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ili amani, upendo na ucha Mungu vistawi duniani.

TOVUTI YETU: www.alislam.org.

**Taarifa za kituo chetu cha**

**MUSLIM TELEVISION AHMADIYYA (MTA)**

ambacho kinafanya kazi muda wote ni:-

**MTA FREQUENCY-12015.V**
**SYMBOL RATE - 29,950**
**SAT SES.5**

**Anuani :-**
Ukiwa na maswali zaidi unaweza kuwasiliana na wabashiri wetu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya nchini kote, kwa:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Arusha/Kilimanjaro | 0787 770 655 |
| 2. | Dar es Salaam | 0655 105 096 |
| 3. | Dar es Salaam | 0620 124 768 |
| 4. | Dodoma/Singida | 0782 919 298 |
| 5. | Iringa | 0715 884 800 |
| 6. | Kagera | 0716 682 063 |
| 7. | Kigoma | 0716 045 918 |
| 8. | Mara | 0785 676 614 |
| 9. | Mbeya | 0714 266 800 |
| 10. | Morogoro | 0714 601 191 |
| 11. | Mtwara / Lindi | 0656 116 652 |
| 12. | Mwanza | 0788 677 509 |
| 13. | Pwani | 0623 228 033 |
| 14. | Shinyanga | 0788 676 618 |
| 15. | Songea | 0656 116 698 |
| 16. | Tabora | 0788 677 433 |
| 17. | Tanga | 0714 583 380 |
| 18. | Tunduru | 0655 028 203 |
| 19. | Zanzibar | 0675 321 543 |

لا اله الا الله محمد رسول الله

**Hapana Apasaye kuabudiwa ila Allah**
**Muhammad ni Mtume wa Allah**

# TUSIWAKASHIFU VIONGOZI WATAKATIFU WA DINI ZOTE

**Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**
**P.O. Box 376, Dar es Salaam.**
**Mnazimmoja, barabara ya Bibi Titi.**
**Mkabala na Bustani ndogo ya Mnazimmoja**
**Email: ahmusjamtaz@gmail.com**

**Imechapishwa na:**
**Ahmadiyya Printing Press Tanzania**
**Mob: 0715 771 813**
**Email: ahmadiyyaprintingpresstz@gmail.com**

بسم الله الرَّحمن الرَّحيم

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu***

# TUSIWAKASHIFU VIONGOZI WATAKATIFU WA DINI ZOTE

Tafrani na zahama kubwa ziliibuka kutokana na vitendo hasi vya baadhi ya waandishi wa habari kuchapisha ndani ya vyombo vyao vya habari picha za vikatuni walivyomnasibisha navyo Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. Hasara kubwa ya mali ilitokea iliyosababishwa na watu walioandamana kulaani kashfa na udhalilishaji huo wa mtu anayeheshimika na mabilioni ya watu duniani. Damu ilimwagika na wengi walijeruhiwa. Na hivi karibuni magaidi wakaivamia ofisi ile ya habari iliyochapisha katuni zile na kufanya mauaji ya kutisha yaliyolaaniwa duniani kote.

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya imekuwa tangu awali ikishauri watu wajiepushe na hali kama hizo ambazo ni tishio kubwa sana la amani. Mnamo tarehe 17 June 1928, Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya wa wakati huo, Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. alitoa nasaha zifuatazo katika mkutano wa hadhara uliofanyika huko Qadian, India. Alisema:

“......Ziheshimiwe nchini mwetu hisia na mienendo ya wengine, ambapo bila ya hizo, Mungu hawezi kupatikana wala amani haiwezi kushamiri duniani. Mafundisho tuliyopewa ndio haya kwamba, tuwaheshimu watakatifu na viongozi wa dini zote. Watu wote wale ambao kaumu zao zinakiri kwamba wao walisimamishwa na Mwenyezi Mungu, watu wote wale ambao Jumuiya zao zina wafuasi wanaokiri kwamba viongozi wao ni mitume wa Mungu au waliotumwa na Mungu ............., tunalazimika kuwaheshimu na kujiepusha kuwakashifu. Na chini ya fundisho hili, sisi daima tumekuwa tukiwaheshimu watakatifu wa kaumu mbali mbali na waanzilishi wa dini zao. Sisi tuna adabu kwa watakatifu wa Wayahudi, tunawaheshimu watakatifu wa Wakristo, tunawatazama kwa mtazamo wa heshima watakatifu wa Wachina. Tunawaheshimu watakatifu wa Wajapani na tunawatukuza hata watakatifu wa Wahindu waliomo nchini mwetu na tunafanya hivyo chini ya agizo la Mwenyezi Mungu. Hatufanyi hayo kwa ubinafsi, hatufanyi kwa kuamriwa na nafsi zetu. Bali sisi twafanya hivyo tukiwaelewa kuwa wao ni wale waliotumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu tukiwafahamu kuwa ni waliotumwa duniani. Nasi twafahamu kwamba watu wa kila kaumu na dini, watakapolitafakari suala hili kwa uaminifu, basi watalazimika kukiri kwamba kustawi kwa dunia, kuwe kwa kiroho au kwa kimwili, kupo katika hali hii kwamba mawazo yetu na kauli zetu ziwe chini ya udhibiti fulani na tuongee kwa njia hii kwamba kusizalike mfarakano na mtengano.

“.............Kwa hakika kuziona sifa za mwingine kunatoa ushuhuda wa uono, na kutoweza kuziona sifa (hizo) ni alama ya upofu. Na Islamu inatuagiza kwamba msiukatae uzuri wa yeyote na muwaheshimu na kuwakirimu viongozi wa dini zingine.

“............njia ya kuukomesha ule mfarakano unaozidi kuongezeka baina ya Wahindu na Waislamu ni hii, kwamba ifanyike mikutano isiyokuwa na mitazamo ya kidini kuhusiana na Mtume s.a.w. bali iwe yenye mielekeo ya kielimu. Kama watu wanaweza kuona na kusikia sifa njema za viongozi wa dini zingine, sasa ni kwa sababu gani wao wasiweze kuziona sifa njema za Mtume Muhammad s.a.w.? watu wasio waislamu pia wanaweza kushiriki kwenye mikutano ya aina hiyo na kwa njia hii, ufa ule unaozidi kuongezeka siku hadi siku unaweza kutoweka na suluhu kuweza kupatikana baina ya Wahindu na Waislamu.

Mbali na hayo, hata Waislamu wenyewe pia, kwa kuzifahamu hali (za maisha) za Mtume s.a.w., imani madhubuti na uaminifu waweza kuzalika (kati yao). Kisha watu wa dini zingine nao watakaposikia hali zake (za maisha) zilizo sahihi, basi watu hao wanaomtusi Mtume s.a.w. wataacha kufanya hivyo.”

“Mapigano mengi husababishwa na mwelekeo huu kwamba watu huzifahamu dini za wengine kuwa ni za uongo na hudhani kwamba; mbali nasi, Mwenyezi Mungu Hajawahi kumpenda yeyote yule mwingine. Watu wengine wote, tangu azali, ni watu waliofukuzwa kutoka kwenye kizingiti cha Mwenyezi Mungu. Sasa dhana hii inapingana kabisa na hali ya asili. Awe mtu wa kaumu yoyote ile au wa nchi yoyote, humfahamu Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye haki ya aina hii hii kwake kama vile ajifahamuvyo mtu mwingine yeyote. Hivyo aisikiapo rai ya aina hii kutoka kwa mtu wa kaumu nyingine, basi huibukwa na jadhba yenye chuki na kuzalika ugomvi na vurugu. Hapo Mtume Muhammad s.a.w. akaufunga kabisa ugomvi huu baada ya kutangaza hivi kwamba;

Yaani hakuna kaumu yoyote ile ambamo hakupita humo nabii. Kwa njia ya tangazo hili, umekubaliwa utakatifu wa manabii wa kila kaumu na chuki ile isababishwayo na ufinyu wa mduara wa kuongoka, huondoka kwenye mioyo ya wale wenye kulizingatia tangazo hili, kwa sababu yeye hufahamu kwamba asili ya dini zote ni ukweli. Hivyo juu ya kuwepo tofauti bado tunaungana. Dini zote zilisimamishwa na Mwenyezi Mungu na ziliendelezwa Naye, hivyo kuzibughudhi na kuzikataa moja kwa moja inakuwa ni kuikataa fadhili yenyewe ya Mwenyezi Mungu. Sasa hebu tafakari jinsi alivyoieleza njia nzuri ya